TANGAZO LA SERIKALI Na. 583 la tarehe 12/7/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1)(b) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA HUDUMA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA ZA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka, 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga;

"hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo katika mwaka husika wa mapato;

"hesabu za mwisho" maana yake ni taarifa za kihasibu zinazowasilishwa na mlipa ushuru baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, zikijumuisha nyaraka, hesabu au maelezo yoyote yanayohusu kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizouzwa;

Sura ya 212

"kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni;

"kipindi maalum cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara yake kwa Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"mlipa ushuru wa huduma" maana yake ni kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara anayefanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa na kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara ambaye mauzo yake kwa mwaka ni zaidi ya shilingi milioni nne kutokana na huduma na miundombinu ya umma anayopata na anayotumia katika kumuwezesha kufanya biashara hiyo katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri husika.

Utozaji wa ushuru

4. Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3) ya mauzo baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa kutoka kwa mtu yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha retani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Muda wa kulipa

5. Bila kuathiri masharti ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na sheria nyingine yoyote, kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha hesabu za awali na kulipa ushuru unaotakiwa katika kila kipindi cha miezi mitatu katika mwaka wa fedha wa Serikali.

Wajibu wa mlipa ushuru wa huduma

6. (1) Kila mlipa ushuru wa huduma atakuwa na wajibu wa-

(a) kulipa ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii ndani

ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi;

(b) kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa sahihi za mauzo;

(c) kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mitatu tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu;

(d) kutunza kumbukumbu za hesabu; na

(e) kutoa kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) (a), Halmashauri inaweza kukubaliana na mlipa Ushuru wa Huduma utaratibu wa kulipa ushuru huo.

(4) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha husika na ametakiwa kufanya hivyo kwa notisi ya siku thelathini, Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa anaweza, kwa kadri atakavyoona inafaa, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(5) Ushuru uliotathminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii utalipwa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

Mamlaka ya mkurugenzi

7.-(1) Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala anaweza-

(a) kukubali hesabu za mwisho na kutathmini ushuru

(b) kukataa hesabu za mwisho na kufanya tathmini ya hesabu iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hesabu zilizowasilishwa siyo sahihi

(c) katika muda wa kazi kuingia kwenye jengo au eneo la biashara la mlipa ushuru kwa nia ya kufanya ukaguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa nyingine kama atakavyoona inafaa kufanyiwa ukaguzi kwa ajili ya kujua kiwango sahihi cha ushuru kinachotakiwa kulipwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza, kwa notisi, kumtaka mlipa ushuru kuwasilisha kumbukumbu za kibiashara na vitabu vya hesabu ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi hiyo, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanya tathmini au kukusanya ushuru wa huduma.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa mashartiya kanuni ndogo ya (2), Mkurugenzi anaweza kumtaka mlipa ushuru kufika mbele yake.

Makosa na adhabu

8. Mtu ambaye-
(a) atashindwa kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa sahihi za mauzo ndani ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) atawasilisha kwa Halmashauri taarifa zisizo sahihi;
(c) atashindwa kulipa ushuru wa huduma katika muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(d) atamshawishi mlipa ushuru wa huduma kukataa au kukwepa kulipa ushuru; au
(e) atamzuia afisa mwidhiniwa au wakala wa Halmashauri kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hii; au
(f) atatoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu suala lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa ushuru,

atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Ufifilishaji wa kosa

9.-(1) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo hii kuhusiana na adhabu, Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu atakaye kiri kutenda kosa kiasi cha Shilingi laki mbili.

(2) mtu atakaye kiri kosa chini ya kanuni ndogo ya (1) atajaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali.

________

JEDWALI LA KWANZA

________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9 (2))*

________

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………. mwenye Simu Na.…………………….. wa S.L.P ……………………….…...ninayefanya biashara……………………………….. katika eneo la ……………………….. lililopo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, kwa hiari yangu mwenyewe nakiri kuwa tarehe………mwezi………… Mwaka…………. nilikiuka masharti ya kanuni ya…………………………...…… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2024.
Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yeyote nakubali kulipa kiasi cha shilingi laki mbili badala ya kushtakiwa Mahakamani na nipo tayari kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu
Jina…………………………………………………………………….
Saini:…………………………Tarehe: ……………………………

MBELE YANGU:
Jina:……………………………………………………………………
Saini:………………………………………………………………….
Wadhifa:……………………………………………………………… 
Tarehe:………………………………………………………………

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ulioitishwa na kufanyika tarehe 1/3/2023 na muhuri wa Halmashauri ilibandikwa mbele ya:-

MWAJUMA A. NASOMBE,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

MHE. Dr. SALEHE R. MKWIZU,
Mwenyekiti,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
WAZIRI wa NCHI OR-TAMISEMI,